**HOTUBA YA MHE. CAPT. WILLIAM P. GUMBO, MSTAHIKI MEYA WA MANISPAA YA MUSOMA ALIYOITOA WAKATI WA UFUNGUZI WA MKUTANO MKUU WA 32 WA JUMUIYA YA TAWALA ZA MITAA TANZANIA (ALAT) KATIKA UKUMBI WA BISHOP JOHN RUDIN TAREHE 22.09.2016.**

Mhe. Dr. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;
Mhe. Menyekiti wa ALAT Taifa;
Mhe. George Simbachawene,(Mb) Waziri Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa;
Dr. Abrahamani Shamumoyo, Katibu mkuu wa ALAT Taifa;
Mhe.Dr. Charles Mlingwa, Mkuu wa Mkoa wa Mara;
Mhe. Dr. Vicent Anney Naano, Mkuu wa Wilaya ya Musoma;
Mabalozi na wawakilishi wakazi wa mashirika ya Kimataifa;
Wajumbe wa Mkutano Mkuu wa ALAT;
Wageni waalikwa;
Mabibi na Mabwana;

Asalaam Alekum!

Naomba nianze kutumia fursa hii adhimu kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa Rehema, kwa kutujalia uzima na kutuwezesha kukutana katika mkutano huu mkuu wa 32 wa Jumuiya ya Tawala za Mitaa Tanzania (ALAT) unaofanyika kwa mara ya kwanza katika mkoa wetu wa Mara hususani Manispaa ya Musoma.

Aidha, napenda kukushukuru wewe mheshimiwa rais kwa ukubali wako kuja kutufungulia mkutano huu bila kujali ratiba ngumu uliyonayo katika kutekeleza majukumu mengine ya kitaifa, ahsante sana. Vilevile, nikupongeze kuchaguliwa kuwa rais wa awamu ya tano wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.Ushindi ulioupata unadhihirisha imani kubwa waliyonayo watanzania kwako.

Kwa namna ya pekee naomba kuushukuru uongozi wa ALAT Taifa pamoja na wajumbe wa mkutano mkuu wa ALAT kwa busara zao na uungwana waliouonesha kuridhia kwa kauli moja mkutano mkuu wa 32 wa ALAT kufanyika mkoa wa Mara, Manispaa ya Musoma.Napenda kuwathibitishia kuwa tumepokea heshima mliyotupatia kwa unyenyekevu mkubwa na tutaendelea kuienzi.

Mwisho lakini si kwa umuhimu napenda kulishukuru kanisa Katoliki jimbo la Musoma kwa upendo wao wa pekee kukubali ukumbi na majengo yao kutumika katika shughuli za mkutano huu. Tumekuwa pamoja bega kwa bega kuhakikisha mkutano huu unafanikiwa. Mungu awabariki sana.

**Mhe. Mgeni rasmi;**
**Mabibi na Mabwana;**

Baada ya shukrani na pongezi hizo niruhusu sasa nitoe ukaribisho wa pekee kwako na kwa wajumbe wote wa mkutano mkuu wa 32 wa ALAT katika Manispaa yetu ya Musoma.Karibuni sana.
Ni ukweli uliodhahiri kuwa Musoma ni mji wenye historia ya kujivunia, mji wa watu waungwana, wenye staha na wanaopenda wageni. Ukweli huu umeendelea kudhihirika mara zote tunapofikiwa na ugeni wa kitaifa kama huu, ni imani yangu kuwa utamaduni huu uliotukuka wa watu wetu utaendelezwa kwa kipindi chote cha mkutano huu.

Mkoa wetu hususani Manispaa ya Musoma imejaliwa kuwa na fursa nyingi ambazo zikiendelezwa vizuri zinaweza kuinua pato la taifa katika sekta za kilimo, utalii, viwanda, Mifugo na usafirishaji.Hivyo kupitia mkutano huu tunawakaribisha wawekezaji na wabia mbalimbali katika kuendeleza mkoa wetu na Taifa letu kwa ujumla.

Kwa mfano katika sekta ya usafirishaji na uchukuzi tunayo bandari ya Musoma inayoweza kutumika kama kiungo muhimu kwa bidhaa zinazosafirishwa kwenda nchi jirani ya Uganda na maeneo mbalimbali. Ombi letu mheshimiwa rais ni kuomba uharakishwaji wa uboreshaji miundombinu ya bandari ya Musoma na ujenzi wa reli.

**Mhe. Mgeni rasmi;**
**Mabibi na Mabwana;**

Bado zipo changamoto nyingi katika ukuaji wa Mkoa wetu ambao una historia ya pekee katika taifa letu, mathalani katika sekta za miundombinu, afya na viwanda.Pamoja na ukweli kwamba ziko fursa nyingi zinazoweza kuharakisha maendeleo yetu bado tunakinzwa na sababu nyingi ikiwemo ukosefu wa fedha za kutosha kugharimia miradi mbalimbali.

Bado nina imani kwamba kupitia ari na kiu kubwa uliyonayo katika kuliletea taifa letu maendeleo na kwenda katika uchumi wa viwanda ni wazi kuwa katika jitihada hizo Mara na hususani Manispaa ya Musoma itapewa nafasi ya pekee.

Hapa kwetu kuna msemo kuwa "Fursa isipotumiwa vizuri inavia" nimeona niitumie fursa hii kujaribu kueleza matamanio ya mkoa na Manispaa yetu kwa sababu inaweza ikachukua muda mrefu kuipata tena, na hata ikipatikana inaweza kuwa tofauti sana na hii ya leo.

**Mhe. Mgeni rasmi;**
**Mabibi na Mabwana;**
Kupitia kauli mbiu ya mkutano wa mwaka huu inayosema "Halmashauri zisipowezeshwa kwa rasilimali utekelezaji wa malengo endelevu ya dunia na agenda ya miji

hautowezekana” Ni uthihirisho tosha wa namna Tawala za serikali za mitaa zilivyo muhimu katika kufikia malengo ya Kitaifa na kimataifa. Ombi langu la pekee kwako ni kuwa serikali na wadau wa maendeleo wataendelea kusaidia kupunguza sana changamoto zinazozikabili mamlaka zetu za serikali za Mitaa kwa kuziongezea uwezo wa vyanzo vya mapato na uwezo wa kujitegemea kwa kuzijengea uwezo.

**Mhe. Mgeni rasmi;**
**Mabibi na Mabwana;**
Nilipewa nafasi hii kuwasalimia wajumbe wa mkutano mkuu na kuwakaribisha katika Manispaa yetu ya Musoma.Nirudie tena kuwakaribisha sana katika Manispaa yetu ya Musoma, tumieni ipasavyo fursa zote tulizonazo katika Manispaa ya Musoma kwa kipindi chote cha mkutano. Kwa upande wetu tutafanya kila linalowezekana kuhakikisha kila mjumbe anafurahia ukarimu wa mji wetu.

Naomba tufanye zoezi dogo kabla sijahitimisha hotuba yangu. Nikisema Mara! Wote tutaitikia Imara!

Mungu Ibariki Mara.
Mungu Ibariki Tanzania.

Ahsanteni sana kwa kunisikiliza.